**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA KILIMO**

**MAMLAKA YA AFYA YA MIMEA NA VIUATILIFU TANZANIA (TPHPA)**

TPHPA
TANZANIA PLANT HEALTH AND PESTICIDES AUTHORITY

**11 Septemba, 2024**

# TAARIFA KWA UMMA

## TARATIBU ZA KUFUATA ILI KUSAFIRISHA PILIPILI KWENDA CHINA

Wizara ya Kilimo inawataarifu wazalishaji na wasafirishaji wa zao la Pilipili kuwa imekamilisha taratibu za kufungua soko la zao hilo nchini China. Kuanzia tarehe 06 Septemba, 2024, Pilipili inayozalishwa nchini imeruhusiwa rasmi kusafirishwa na kuuzwa katika soko la China.

Ili Msafirishaji aweze kuuza Pilipili nchini China anatakiwa kusajiliwa na Mamlaka ya Forodha ya nchini China (General Administration of Customs of China – **GACC**) kupitia Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (Tanzania Plant Health and Pesticide Authority - TPHPA). Pamoja na kusajiliwa, Msafirishaji anapaswa kuzingatia matakwa yafuatayo:-

i. Aina ya Pilipili zinazokubaliwa nchini China ni jamii zote za Pilipili ikiwa ni mbichi au iliyokaushwa;
ii. Mashamba ya uzalishaji na maeneo ya ufungashaji (packhouse) yanapaswa kusajiliwa na Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) na kupewa namba maalumu ya utambulisho itakayotumika kumtambulisha Msafirishaji;
iii. Mashamba yote yaliyosajiliwa kwa ajili ya kusafirisha Pilipili kwenda China yanapaswa kuzingatia mbinu bora za kilimo pamoja na udhibiti husishi wa visumbufu vya karantini ikiwemo nzi wa matunda, vidomozi vya majani na magonjwa ya kutu na mnyauko yanayosababishwa na vimelea vya Bakteria;
iv. Uchakataji, ufungashaji, uhifadhi na usafirishaji lazima uzingatie matakwa na taratibu zote zilizoko kwenye itifaki tuliyosainiana kati ya Tanzania na China na utekelezaji wake utasimamiwa na TPHPA.

Mawasiliano zaidi kuhusu taratibu za usajili tuandikie kupitia barua pepe phbi@tphpa.go.tz au tembelea tovuti yetu https://www.tphpa.go.tz.

Imetolewa na,

Prof. Joseph C. Ndunguru
**MKURUGENZI MKUU**